MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI 2022

Na Abdallah Mahia (04 Juni, 2022)

Maadhimisho ya siku ya mazingira Duniani huadhimishwa kila tarehe 5 mwezi wa Sita kila mwaka, lakini bado kumekuwepo na changamoto kadhaa kama vile kuharibika kwa mifumo ya ikolojia ambako kumesababisha madhara makubwa ikiwemo ukataji miti holela, utiririshaji maji machafu kwenye mito, maziwa, sambamba na utoaji gesi joto kutoka kwenye mitambo mbalimbali viwandani na vyombo vya usafiri.

Katika kufikia dira na dhima ya kufanya tahmini ya athari kwa mazingira na kukuza uelewa kwa wananchi kuhusu mazingira, kuratibu shughuli za usimamizi wa mazingira na kufanya tafiti za mazingira ili kuongoa mifumo hiyo. Hali kadhalika uharibifu wa mifumo ya ikolojia unahatarisha sana biashara ambapo mifumo hii ikiharibika inaharibu uchumi, na kwa sasa dunia imekuwa ikikabiliwa na majanga haya ya uharibifu wa mifumo hii ya Ikolojia.

Aidha mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanasababisha mvua zisizo na mpangilio, ongezeko la joto, kuharibika kwa miundombinu sambamba na kuongezeka kwa kina cha maji kwenye bahari na maziwa.

Jukumu la utunzaji wa mazingira ni la kila mtu, na hakuna dunia nyingine zaidi ya hii, hivyo ni wajibu jamii ikatunza mazingira yetu kwa ustawi wa afya na maendeleo endelevu.

Kwa upande wa usimamizi wa usafi wa mazingira katika jamii kwa ngazi za Halmashauri za Mamlaka za miji, Wilaya, Manispaa na majiji ni suala linalotakiwa kuwa sehemu ya maisha ya watu wote kila siku na mara kwa mara yaani tabia. Haitakiwi kusubiri hadi tamko litolewe na mamlaka za juu ndipo watu wakumbuke umuhimu wa usafi katika maeneo yao.

Pamoja na mafanikio tuliyo nayo, tunahitaji kuhakikisha tunaendeleza utaratibu huu kuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku kwamba usafi ufanyike kila mara na si kusubiri matamko ya viongozi wa juu.

Udumishwe utaratibu wa kutekeleza sheria katika mitaa tunayoishi kwamba usafi usimamiwe kikamilifu kwa wanajamii bila jukumu hilo kuziachia mamlaka za serikali pekee ili kuhakikisha kuwa tunafanikiwa.

Ile sheria ya "atupaye taka ovyo aadhibiwe", iendelee kutekelezwa kwa vitendo bila kuhusisha masuala ya kisiasa, endapo baadhi watabainika kukiuka sheria hiyo hatua zichukuliwe bila kujali hadhi au aina ya mtu katika jamii iwe kiongozi, mtu maarufu au mwananchi wa hali ya chini ili kuendeleza muonekano mzuri wa mandhari ya mazingira yetu.

Abiria waelimishwe juu ya utunzaji wa mazingira, wasichafue mazingira kwa kisingizio cha safari, sheria zitumike kwa wasafiri husika na wamiliki wa vyombo hivyo. Ile dhana ya "kuchimba dawa" itakuwa historia.

MaAfisa Afya wa mtaa waonekane katika mitaa wakisisitiza usafi pamoja na kuihamasisha jamii kupenda usafi kwa dhati ya mioyo yao.

Pia kutengwe maeneo maalum ya ujenzi wa vyoo kwa wasafiri na ya kutupia taka katika mitaa, ni muhimu kwa yale maeneo ya halmashauri ambazo hazijafanya hivyo pia yawekwe mabango na matangazo yanayokataza kutupa taka ovyo ikionyesha na vifungu vya adhabu kwa atakayekiuka, kwani hii itapunguza watu ‘kuchimba dawa’ na kutupa taka ovyo katika vichaka, mitaro, barabara, vichochoro na kwingineko.

Aidha, Serikali itenge bajeti na kuweka kipaumbele katika afya ya mazingira kitakachozingatia kila halmashauri kuwa na magari ya kutosha ya kubebea taka ikiwamo ujenzi wa madampo makubwa na ya kisasa katika kila halmashauri.

Halmashauri zitakazoshindwa kujiendesha zifanye mpango wa utoaji wa zabuni kwa kampuni zinazohusika na uzoaji wa taka na kufanya usafi hususan katika miji mikubwa na uwe ni wa ushindani kwa kushirikisha kampuni mbalimbali.

Tuepuke kampuni ambazo hazina vifaa vya kutosha huku baadhi ya wafanyakazi wakikosa hata vifaa vya usafi kama vile koleo, fagio, mask, matoroli, reki na matoroli ya kubebea taka.

Kwa kuwa miji yetu inakua kwa kasi kubwa ufike wakati miundombinu ya huduma za kijamii iendane na kasi hiyo ili afya za wananchi ziwe bora.

Majengo makubwa, migahawa na maeneo ya soko ambayo huzalisha taka ngumu kila siku yawe na uwezo na wapewe utaratibu wa kutunza taka hizo na mamlaka husika.

Katika majiji makubwa kama Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Tanga changamoto kubwa ni kasi ya ongezeko la idadi ya watu wanaozalisha tani elfu za taka kila siku, kusikoendana na ukusanyaji wa taka hizo. Hii iwe mfano kwa miji inayokua kupanga mji mapema (urban & town planning).

Na iwe ni wakati wa kujifunza kutoka kwa baadhi ya wenzetu (Halmashauri na majiji) wanaotunza maeneo yao, na wataalamu waliopo nchini watumiwe ipasavyo ili kutoa ushauri wa namna ya kukabiliana na uchafu.

Jitihada hizi pamoja na kuungwa mkono na wananchi, raia wa kigeni (Donors), haitatosha iwapo wanasiasa watahusika kwa utetezi wa wapiga kura wao watakaochafua na kuharibu mazingira maana hakuna mikakati itakayoweza kutekelezeka ya kuuendeleza usafi huo katika maeneo yetu ikiwamo kutokomeza magonjwa mbalimbali na hasa yale ya mlipuko kama wanasiasa wataegemea kwa wachafuzi na waharibifu wa mazingira.

"Hakuna lisilowezekana"

Abdallah Mahia ni Afisa Afya wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma.